

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**



**TANGAZO KWA UMMA**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uthibitishwaji wa Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano, Usuluhishi na Upatanishi, za mwaka, 2021 (*the Reconciliation, Negotiation, Mediation and Arbitration (Practitioners Accreditation) Regulations, 2021*) imetoa sharti la ukomo wa muda wa cheti cha usajili wa Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano, Usuluhishi na Upatanishi kuwa ni miaka miwili (2). Pia kwa mujibu wa Kanuni ya 18 ya Kanuni za Uthibitishwaji wa Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano, Usuluhishi na Upatanishi za mwaka, 2021 imetoa mamlaka kwa Msajili wa Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano, Usuluhishi na Upatanishi, baada ya kupokea maombi ya Mleta Maombi, kuhuisha Cheti chake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni tajwa hapo juu.

Hivyo basi, Wizara inapenda kuwatangazia Watoa Huduma za Usuluhishi, Upatanishi, uendeshaji wa maridhiano na Majadiliano ambao vyeti vyao vimefikia ukomo wa muda, kuhuisha vyeti vyao kwa mujibu wa Sheria. Waleta Maombi watapaswa kujaza fomu ya maombi TAF3 iliyopo kwenye Kanuni za Uthibitishwaji wa Watoa Huduma za Maridhiano, Majadiliano, Usuluhishi na Upatanishi za mwaka, 2021, pamoja na kuwasilisha nyaraka zifuatazo;

- i) Nakala ya Cheti kilichoisha muda wake
- ii) Fomu ya tamko la maadili (declaration form)
- iii) Wasifu (CV) ili kupata maboresho ya wasifu husika
- iv) Vyeti vya taaluma ambavyo havikuwasilishwa awali kama vipo

Kwa muktadha huo, Wizara ya Katiba na Sheria inawatangazia watalaam wote na mashirika yote ambao vyeti vyao vya usajili vimeisha muda kuhuisha vyeti vyao ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya uendeshaji Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi kwa tozo/ada hapa nchini. Kwa kuwa Wizara inaboresha mfumo wa usajili kwa sasa maombi hayo na viambatisho viwasilishwe kupitia barua pepe ya [msajili.mmuu@sheria.go.tz](mailto:msajili.mmuu@sheria.go.tz) endapo kuna maombi changamoto yoyote tafadhali wasiliana na Msajili kupitia namba yake yake simu 0629527794.

Pia, Wizara imebaini wakati wa upokeaji wa maombi haya baadhi ya Waleta Maombi wamekuwa wakilipa ada kubwa tofauti na ada iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Wizara inawakumbusha Waleta Maombi ya kuhuisha vyeti kulipa ada kwa mujibu wa Kanuni za Ithibati ya Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi, za mwaka, 2021 (the Reconciliation, Negotiation, Mediation and Arbitration (Practitioners Accreditation) Regulations, 2021.

#### **Ada ya Usajili (Accreditation Fees)**

<b>Na.</b>	<b>Kada</b>	<b>Kiasi</b>
1.	Upatanishi(mediation)	100,000/=
2.	Usuluhishi(Arbitration)	300,000/=
3.	Majadiliano(negotiation)	100,000/=
4.	Maridhiano(reconciliation)	100,000/=

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI  
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA  
20Juni, 2023**